



UZALISHAJI WA MICHE YA NANASI KWA KUTUMIA TEKNOLOJIA YA CHUPA (TISSUE CULTURE)

Utangulizi

- Nanasi (*Ananas comosus* (L.) Merr.) ni moja ya zao la matunda ya kibiashara linaloongoza katika ukanda wa Kitropiki, na ina nafasi muhimu sana katika uchumi wa nchi nyingi.
- Ni chanzo cha vitamin A na B, na kuwa na kiasi kikubwa cha vitamin C pamoja na madini .
- Hata hivyo, pamoja na umuhimu wake, uzalishaji nchini Tanzania bado hauridhishi kwani matunda yanayovunwa hutofautiana kwa ubora na ukubwa, na hivyo upatikanaji wa soko kuwa mgumu.
- Uzalishaji wa matunda yasiyo na ubora unachangiwa zaidi na ukosefu wa mbegu zilizo bora, mbinu bora za kilimo kwa ajili ya uzalishaji wa kibiashara, na uwepo wa wadudu waharibifu na magonjwa.
- Hivyo, teknolojia ya kuzalisha miche katika maabara kwa njia ya chupa imeonekana ni mkombozi kwa mazao ambayo yana uhaba wa mbegu au upatikanaji wa mbegu ni mgumu.



HATUA ZA UZALISHAJI WA MICHE YA NANASI KWA NJIA YA CHUPA KATIKA MAABARA

Hatua ya 1. Maandalizi ya mbegu mama (mother stock)

- Ukusanyaji wa mbegu mama (crown) kutoka kwenye tunda la nanasi lililokomaa.
- Uondoaji wa majani na usafishaji wa mbegu mama kwa kutumia dawa (disinfectant) katika eneo maalum (Lamina Flow cabinet).



Nanasi lililokomaa lenye mbegu mama



Mbegu mama



Uondoaji wa majani na usafishaji wa mbegu mama

Hatua ya 2. Uzalishaji



Mbegu mama kwenye kirutubisho



Utengenezaji wa vichipukizi



Kupanda miche kwenye shamba



Kuizoeha mimea mazingira ya nje na maabara



Utengenezaji wa mizizi

Faida ya kuzalisha miche ya nanasi kwa kutumia njia ya chupa katika maabara Miche yote inafanana na mbegu mama.

- Miche mingi inaweza kuzalishwa kwa muda mfupi.
- Inapatikana miche bora na isiyokuwa na magonjwa wala wadudu.
- Miche inaweza kuzalishwa kwa mwaka mzima kulingana na uhitaji wa wakulima pamoja na wadau wengine wa kilimo.
- Inasaidia kuongeza kasi ya uzalishaji wa miche ya nanasi kwa ajili ya wakulima wadogo pamoja na wakubwa.

